

Uhusiano wa Sera ya Kielimu na Maendeleo ya Kiswahili Nchini Uganda kwa Kuegemea Nadharia ya Uchaguzi na Utekelezaji wa Lugha

Masereka Levi Kahaika
Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda

Ikisiri

Uganda ni nchi mojawapo iliyomo katika jumuiya ya Afrika Mashariki ambako Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kutokana na kifungo 137 cha katiba ya jumuiya. Nchini Uganda kumekuwepo maandiko mengi kuhusiana na matumizi ya Kiswahili katika taasisi za kielimu ikiwa ni pamoja na ripoti ya Kajubi ya 1987, *Government White Paper on Education* ya 1992 pamoja na CURASSE¹ ya 2013 iliyopendekeza Kiswahili kuwa lugha ya lazima katika shule za msingi na za upili nchini kote. Pamoja na mapendekezo hayo yote, vyuo vyote vya taifa pamoja na vya kibnafsi vilichukua jukumu la kufundisha walimu ambao wamehitimu katika kufundisha Kiswahili katika viwango vyote vya kielimu. Pamoja na kuweco kwa walimu ambao wamehitimu kupitia vyuo hivyo, serikali haijatekeleza suala la kufanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za msing na upili. Kwa kuongozwa na nadharia ya uchaguzi na utekelezaji wa lugha pamoja na nadharia ya upangaji lugha, makala haya yanabainisha uhusiano wa sera ya kielimu na maendeleo ya Kiswahili ilivyo nchini Uganda na kupendekeza njia za kuinua hali hiyo. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa matini zilizoandikwa kuhusu Kiswahili.

Maneno Muhimu: Sera, Kiswahili, Elimu, Lugha, Uganda

Utangulizi

Ikumbukwe kuwa kufikia mwaka 1987, kwa miaka 32 mfumo wa elimu nchini Uganda ulikuwa unaendelezwa kufuatana na mapendekezo ya *Castle Education Commission* ya 1963 (Mukama 2009). Vilevile, kumekuweco sheria nyingi za kielimu ambazo zinazungumzia ufundishaji wa Kiswahili tangu enzi za ukoloni kuanzia miaka ya 1903 wakati ambapo Sir William Gowers aliamuru kwamba Kiswahili kifundishwe nchini

¹ CURASSE: Ni kifupisho cha Curriculum Reform Assessment and Evaluation.

Uganda. Awali ya yote, tume ya *Phelp Stokes* ya 1924-1925 ilikuwa imependekeza ufundishaji wa Kiswahili na kuitumia kama lugha ya kufundishia katika shule za upili. Baada ya hapo kukaja tume ya *de La Warr* ya 1938 ambayo ilipendekeza kwamba badala ya Kiswahili Kiingereza iwe ndiyo lugha ya kufundishia katika shule za msingi (Jjinga na Visser, 2017).

Mbaabu (2007) na Mukama (keshatajwa) wanaeleza kwamba sera ya lugha ya 1952 ilipendekeza kwamba Kiswahili kitolewe katika orodha ya masomo yanayofundishwa nchini Uganda. Mapendekezo haya yalitolewa katika tume ya *Binns* ya 1952. Naye Mpuga (2003) anaeleza kwamba Kiingereza kiliteuliwa kama lugha ya kiutawala baada ya wakoloni kushindwa kujifunza lugha nyingi za Uganda. Kauli hii inapingana na wazo kwamba Tanzania ina makabila mengi lakini wakoloni walijifunza Kiswahili.

Pamoja na kwamba viongozi wa ukoloni walipendekeza matumizi ya Kiswahili kama lugha inayozungumzwa Afrika Mashariki na Afrika ya kati, Kajubi (1987) aliegemeza mapendekezo hayo kwenye maoni hayo katika kutoa ripoti yake kuhusu mfumo wa elimu unaohusisha Kiswahili (Mukama, 2009). Mapendekezo yenyewe yalisitizwa katika sehemu 36:iv ya *Government White Paper on Education* ya 1992 kwamba Kiswahili na Kiingereza yafundishwe kama masomo ya lazima katika mfumo wa elimu nchini Uganda (Nakindu na wenzake, 2015). Vilevile, mapendekezo ya ripoti ya Kajubi (keshatajwa), yalichangia pakubwa katika uanzishaji wa ufundishaji wa Kiswahili katika Chuo cha Kakoba na Kyambogo na baadaye Chuo Kikuu cha Makerere ambako Kiswahili kiliwahi kuanzishwa mwaka wa 1927 na kikasitishwa. Vyuo vingine pia vilianza kukifundisha na shirika la UNEB² likaanza kutunga Mitihani ya Kiswahili kwa kiwango cha kidato cha nne na cha sita (Jjinga na Visser, 2017).

Suala la sera ya lugha na utekelezaji linafaa kuzingatiwa sana ili kuwepo utekelezaji wa masuala ya kiisimu-jamii katika jamii husika. La sivyoyote, hata pakiwepo sera au mpangilio maalum unaohusu lugha bila kutekelezwa vizuri kunaweza kutokea mkanganyiko (Rusekampunzi 1988). Nchini Uganda, kuna mashirika na taasisi mbalimbali zinazohusika na uundaji wa mapendekezo kuhusu na lugha ya Kiswahili. Taasisi hizi ni za kielimu, pamoja na kisiasa. Rusekampunzi (keshatajwa) katika utafiti wake kuhusu sera ya lugha na maendeleo ya Kiswahili nchini Rwanda, ameeleza kuwa kuwepo kwa sera inayoruhusu ujifunzaji wa lugha unasaidia lugha kuendelea kutumiwa katika masuala ya kisiasa, kielimu, kitamaduni, kijamii na kiuchumi. Makala haya yamejadiliwa kwa kurejelea nadharia ya Upangaji lugha, hali ilivyo nchini Uganda, hakuna sera ambayo imethibitisha kufundishwa kwa Kiswahili. Yaliyopo ni mapendekezo ambayo mara nyingi hayatekelezwi. Lengo kuu la makala haya ni kueleza hali ilivyo kuhusiana na Kiswahili na kutoa mapendekezo yanayoweza kuchangia utekeleza wa mapendekezo yanayoshabiki utekelezaji wa Kiswahili.

² UNEB: Ni kifupisho cha Uganda National Examinations Board.

Mapitio ya Maandishi kuhusu Lugha nchini Uganda

Uganda ilipopata uhuru, shirika la radio ya Uganda UBC³, lilikuwa linatangaza habari kwa lugha chache ikiwa ni, Kiingereza, Luganda, Runyoro/Rutooro, Ateso, na Lwo. Lakini mnamo mwaka wa 1967, wakati rais Obote alikuwa anahutubu katika warsha iliyoandaliwa na shirika linalohusika na mambo ya utangazaji Afrika Mashariki (*Mass media and Linguistic Communications in East Africa*), alitangaza kwamba lugha nyingine kumi zingengezewa katika zile zilizokuwa zikitangazwa katika shirika la UBC. Mnamo mwaka wa 1969, lugha nyingine ziliongezewa kutoka lugha kumi zikawa kumi na nane ambazo ni; Kiingereza, Luganda, Lusoga, Lunyole/Lusamia/Lugwe, Lumasaba, Sebei, Runyoro/Rutooro, Runyankole/Rukiga, Lwo, Ateso, Karomojang, Madi, Kakwa, Lugbara, Alur, Kumam na Hindustani. (Nsibambi, 1971). Nsibambi (keshatajwa) anaeleza kuwa rais Obote alisema:

I am in government and I have to take the political feelings of the people into account in formulating policies

Tafsiri: Niko serikalini na wajibu wangu ni kutekeleza masuala ya kisiasa kama inavyotarajiwa na watu kwa kuunda sera” (Tafsiri hii na nyingine zote zitakazofuata ni yangu)

Viera (1996), katika kazi yake, “*Swahili and the Dilemma of Uganda Language Policy*” anaeleza kuwa mbali na kuwa ingawaje Tanzania na Kenya zimepiga hatua kuhusiana na masuala ya lugha hasa Kiswahili, nafasi ya Kiswahili nchini Uganda haieleweki. Anaendelea kueleza kuwa masuala yanayohusu lugha hasa ya Kiswahili yatachukua muda. Madai ya Viera (keshatajwa) yalitolewa sasa miaka ishirini na moja lakini mpaka sasa sera kuhusu Kiswahili haipo na mapendekezo yanayohusu Kiswahili mengi yanabaki kwenye karatasi. Hali hii ilichochea utafiti huu ili kuweza kutoa mchango ambao umependekeza ni kipi cha kufanya ili kuinua Kiswahili nchini Uganda.

Tembe (2008), katika utafiti wake kuhusu sera inayohusu lugha miongoni mwa jamii inayozungumza lugha nyingi nchini Uganda, akirejelea “*Government White Paper on Education*” iliyoongozwa na Kajubi (1992), anasema kwamba endepo mapendekezo yaliyomo yatatekelezwa, mwelekeo wa kiisimu nchini Uganda utabadilika, kiasi cha kuwa Uganda itakuwa katika hali moja na Tanzania na Kenya. Tangu 1992, mapendekezo ya “*Government White Paper on Education*” yamebaki kwenye karatasi kiasi cha kuwepo mapendekezo yanayopingana, mara leo Kiswahili kimeondolewa katika silabasi, mara kitakuwa lugha ya lazima na kuwafanya walimu na wanafunzi pamoja na mashirika ambayo yangeweza kuendeleza Kiswahili kuwa katika hali ya mkanganyiko.

³ UBC: Uganda Broadcasting Cooperation.

Kutokana na Mazrui na Mazrui (1995), kwenye mkutano uliofanyika mwaka 1929 Sir Daudi Chwa mfalme wa Buganda alipinga mapendekezo ya Sir Gowers kwa madai kwamba uendelezaji wa Kiswahili ungepotosha hadhi ya kabila lao na urai miongoni mwa makabila mengine ya Afrika. Hata hivyo, hakupinga ufundishaji wa wake kwa sababu ingesaidia watu wake kupata ajira. Mazrui na Mazrui (keshatajwa) wanaeleza kuwa gavana wa Uganda, Sir W.F. Gowers alipendekeza kwamba Kiswahili kianze kutumiwa katika masuala ya kiserikali na lugha ya kufundishiwa katika shule. Alisema kwamba katika maeneo ambako Kiganda na lugha za kienyezi zilikuwa zinatumiwa alipendekeza kwamba Kiswahili kitumiwa na Kiganda kitolewe. Gavana Gowers alikuwa na ndoto za kuendeleza Kiswahili katika masuala ya Kiswahili. Katika kongamao la 1962 wajumbe walikuwa wanaangalia uwepo wa muungano walipendekeza kuwepo kwa Kiswahili.

Tume ya *Government White Paper on Education* ya 1992 iliyoshughulikia mapitio ya masuala ya elimu nchini Uganda, kwa mada ya “*Education for National Intergration and Development*” ilipendekeza kuwa Kiswahili na Kiingereza yafanywe masomo ya lazima katika shule za msingi. Kama ilivyotajwa awali na Nakindu na wenzake (2015) walipendekeza kwamba somo la Kiswahili lipewe muda wa kutosha kwenye ratiba hata serikali ishiriki katika kutoa vifaa vya kufundishia kwa kuwa Kiswahili ni lugha ambayo ingeunganisha Waganda kama jamii moja na umoja huo ungeleta maendeleo (Mugagga, 2010).

Mapendekezo ya “*Government White Paper on Education*” yalichangia pakubwa katika uanzishaji wa Kiswahili katika baadhi ya shule za upili hasa hasa katika shule za upili za magharibi na hata katika baadhi ya shule za kibinafsi, katika shule za upili katika eneo la Buganda na kusababisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaofanya Kiswahili katika kidato cha nne. Lakini tangu 1992 kumekuwepo upotoshaji wa watu mara Kiswahili kimeondolewa katika silibasi na kusababisha baadhi ya walimu wakuu kuwatimua walimu wa Kiswahili.

Ssekamaanya (2017) aliyefanya utafiti wake kuhusu sababu za idadi ya wanafunzi wanaofanya Kiswahili kupungua katika kidato cha sita, anaeleza kuwa ukinzani kisera ndio ulisababisha upungufu huo. Anaendelea kueleza kuwa, isingelikuwa ukinzani wa kisera kuhusu ufadhili, idadi ya wanafunzi wanaofanya Kiswahili ilikuwa imeanza kuongezeka. Anaeleza kuwa kati ya 2000 na 2005, wanafunzi waliofanya Kiswahili katika mtihani wa mwisho darasa la nne walikaribia elfu ishirini (ripoti ya UNEB 2008). Hata hivyo, miaka mitano baadaye, Serikali nchini Uganda ilipitisha sera ambayo ilibadilisha kutokuwepo malipo ya serekali kwa mwanafunzi yeyote anayesoma masomo ya sanaa katika vyuo vikuu. Sera hii ilianza kuathiri idadi ya wanafunzi wa masomo ya sanaa wakaanza kupungua huku wale wa sayansi idadi ikipanda.

Tangu miaka ya 2006 hadi sasa, Chuo Kikuu cha Kyambogo kilizindua tena ufadhili kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa kiwango cha shahada. Pia mnamo mwaka wa 2010, Chuo Kikuu cha Kyambogo kilianzisha kozi ya Kiswahili na wakaanza kutahiniwa rasmi mwaka 2013. Shirika la NCDC⁴ mnamo mwisho wa mwaka wa 2013, lilitangaza kuwa somo la Kiswahili litakuwa somo la lazima katika shule za msingi na za upili nchini Uganda. Mbali na maendeleo haya kuhusu somo la Kiswahili, idadi ya wanafunzi wanaofanya Kiswahili bado inapunguka na sababu ni kutotekeleza baadhi ya mapendekezo kama itakavyoelezwa kuhusiana hapo chini.

Nadharia na Mapendekezo

Makala haya yamejikita katika nadharia ya Uchaguzi na Utekelezaji wa Lugha ambayo iliasisiwa na Haugen (1966) ambaye alianza shughuli zake mnamo 1959 alipoeleza neno Upangaji Lugha alipokuwa anaeleza juhudi zilizofanywa Norway kutumia lugha kiuzalendo na kibinafsi. Aliendelea kuzungumzia upangaji wa othografia, sarufi, uundaji wa kamusi na kuongoza wazungumzaji katika jamii inayotumia lugha tofautitofauti. Mnamo 1996, Haugen alipendekeza kwamba upangaji lugha ni mojawapo ya matokeo ya upangaji, au utekelezaji wa uamuzi unaofanywa na wapangaji wa lugha. Katika kazi yake ya (1969), Haugen alitoa fasili ya upangaji lugha kwamba ni kuanzishwa kwa malengo, sera na utaratibu wa lugha katika jamii.

Haugen (1966) alieleza hatua nne za Upangaji Lugha ikiwa ni, uteuzi wa kawaida, muundo, utekelezaji na ufafanuzi. Makala haya yalijikita katika uteuzi na utekelezaji. Haugen (keshatajwa) alieleza kuwa uteuzi wa kawaida unahusu uteuzi wa lugha kwa kuteua sheria rasmi inayohusu lugha fulani. Kuhusiana na makala haya, muhimili huu umetufaa kwa kuchunguza ni sheria zipi ambazo zipo au zimewahi kuwepo na zimechangiaje uendelezaji na ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Kufuatana na muhimili huu kama ilivyoelezwa hapo awali, makala haya yalibaini kwamba mbali na kuwa Kiswahili kimependekezewa kama lugha ya kufundishwa katika shule kama somo la lazima, jambo hili limebaki katika makaratasi tu wala utekelezaji umekuwa ni ndoto za hekaya.

Mnamo 2017, gazeti la Newvision tarehe 22 mwezi wa Novemba (gazeti la serikali) lilitangaza kwamba somo la Kiswahili litafanywa somo la lazima nchini Uganda. Taarifa kama hizi zimekuwa zikitokea na wala utekelezaji unakuwa ndoto. Vilevile, Haugen (keshatajwa) alizungumzia juu ya muhimili wa utekelezaji kuwa ni shughuli za taasisi mbalimbali za kibinafsi na za kiserikali katika kutekeleza lugha fulani. Shughuli hizi zinahusu kutumia lugha husika katika shughuli za kijamii, kielimu pamoja na uandikaji wa vitabu. Haugen (keshatajwa) anasema kwamba kutimizwa kwa shughuli hizo anazirejelea kama kukubalika. Ni kutokana na muhimili huu kwamba

⁴ NCDC: Ni kifupisho cha National Curriculum Development Centre (Shirika linalohusika na uandaaji wa mitalaa nchini Uganda).

makala haya yaliangazia mchango wa wizara zinazohusika na masuala ya Kiswahili, ni kipi kinachotarajiwa kufanywa na wizara hizo, na ni kipi ambacho kimefanywa. Aidha, mashirika ambayo yanahusiana na uandaaji wa mitalaa kama NCDC, UNEB ambayo inatahini pamoja na shirika la NCHE⁵ ambalo linahusika na uendelezaji wa masuala ya kielimu kwa kiwango cha vyuo vikuu na vyuo vingine. Makala haya yalibaini kwamba NCDC imewajibika kwa kuandaa silabasi na kupendekeza vitabu ambavyo vinafaa kurejelewa katika kufundishia (Jjinga na Visser 2017). Juhudi za NCDC mara nyingi zimekuwa zikitingwa na serikali kwa kutotekeleza mapendekezo husika. Nalo shirika la UNEB likishirikiana na NCDC limekuwa likitahini mitihani ya Kiswahili kwa kiwango cha kidato cha nne na sita.

Shirika la NCHE kupitia vyuo vya ufundi na kibiashara pamoja na vyuo vikuu limechangia katika kufundisha Kiswahili. Hata hivyo, uwajibikaji wa mashirika haya unahitaji mchango wa serikali kwa kusaidia katika kutoa vifaa. Utafiti uliofanywa ulibaini kwamba hakuna mwalimu ambaye ameajiriwa na serikali kufundisha Kiswahili katika vyuo vya ufundi jambo ambalo linatatiza uendelezaji wa ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo hivyo. Sanjari na hilo, NCHE haijatalia mkazo suala la kukifanya kila chuo kama vya kiafya kufundisha Kiswahili. Hali hii inakiuka mapendekezo ya *Government White Paper on Education* kwamba Kiswahili kinafaa kifundishwe kwa watu wote nchini Uganda ili kuwawezesha kuendeleza umoja.

Baada ya maoni ya Haugen (1966), nadharia iliendelezwa na Kloss (1968). Kloss (keshatajwa), aliongezea mihimili miwili ikiwa ni; Upangaji Lugha kihadhi na Upangaji wa uandishi. Alieleza kwamba upangaji wa uandishi unahusu mabadiliko katika muundo, msamiati, mofolojia na tahajia. Aliendelea kuzungumzia juu ya muhimili wa upangaji lugha kihadhi kwamba ni utambuzi wa lugha na serikali kwa manufaa ya serikali au kuonesha hadhi ya lugha ikilinganishwa na lugha nyingine. Katika makala haya tumeangalia ni jinsi gani serikali ya Uganda imechangia katika kuipa hadhi lugha ya Kiswahili, hadhi hiyo ni ya juu au ni ya chini? Na imechagijaje katika kukiendeleza Kiswahili na utekelezaji wa Kiswahili kielimu.

Kuhusiana na muhimili ulio hapo juu ilibainika kwamba kihadhi na kimaandishi, Kiswahili imepewa hadhi ya juu kwa kurejelea katiba ya nchi iliyoandikwa mwaka 1995 na kufanyiwa marekebisho mwaka wa 2005, katiba inatambua Kiswahili kama lugha rasmi ya pili kama ilivyonukuliwa hapa:

The 1995 National Constitution as amended in 2005, clause 2 of article 6 states that, Swahili shall be the 2nd official language in Uganda.

Tafsiri: Katiba ya kitaifa ya 1995 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005, kifungu cha pili katika ibara ya pili inasemwa kwamba, Kiswahili itakuwa lugha rasmi ya pili nchini Uganda.

⁵ NCHE: Ni kifupisho cha National Council for Higher Education.

Kiutekelezaji, hakuna juhudi hata iwe za kuwafundisha watu au hata raia kutumia Kiswahili au hata kutangaza kuwa itumiwa katika afisi au hata shughuli za kiserikali.

Naye Nahir (2003) anapendekeza malengo kumi na moja kuhusiana na upangaji lugha. Lakini kwa mujibu wa makala haya tumechukua haya hapa chini ambayo tulihisi kwamba yanahusiana na mada ya makala haya, nayo ni kama yafuatayo;

Uratibishaji lugha: Hili linahusiana na kuilinda lugha dhidi ya kuingilia lugha za kigeni na kuilinda dhidi ya uchepukaji lugha kwa kuingiliwa na lugha za kienyeji. Kufuatana na hili makala haya yanaangazia ni kwa jinsi gani lugha za kienyeji nchini Uganda zimeingilia Kiswahili. Makala yanatambua kwamba kumekuweko mwingilio kisera wala si kiisimu pale ambapo Kiswahili kinapopendekezwa na lugha za kienyeji kama Kiganda zinaletwa mezani. Katika baadhi ya shule za upili Kiganda kimependelewa na Kiswahili kufutwa.

Ufufuaji lugha: Mpango huu huwafanya wenyeji kuishikilia mifumo ya lugha hiyo kimawasiliano. Hili limetuongoza katika kutathimini jinsi msimamo hasi nchini Uganda kwamba Kiswahili ni lugha ya wezi umebadilishwa. Kwanza kabisa makala haya yanatambua kwamba Kiswahili kutokana na enzi za rais Amin pamoja na kuwa Kiswahili ilitumiwa na askari wake kukandamiza watu, kwa sababu hii baadhi ya wazazi huwakataza watato wao kujifunza Kiswahili kwa madai kwamba ni lugha ya wezi.

Usambazaji lugha: Msingi huu unalenga kuongezea idadi ya wazungumzaji lugha fulani na kutoendeleza lugha nyingine. Katika makala haya, msingi huu ulitufaa katika kuchunguza mapendekezo ambayo yananiua kuendeleza Kiswahili katika taasisi za kielimu. Makala yalibaini kwamba mbali na kuwa kuna mapendekezo ya kuendeleza na kusambaza Kiswahili nchini Uganda, Kiingereza bado kinatiliwa maanani kuliko Kiswahili. Hili linakwamiza usambazaji wa Kiswahili nchini Uganda.

Kuwezesha mawasiliano kati ya jamii za lugha tofauti: Msingi huu pia umezingatiwa katika makala yetu kwa kuchunguza mikakati inayofanywa na serikali. Lililopo ni kwamba nchini Uganda hakuna lugha ya taifa ingawaje kuna makabila mengi ambayo kwa kweli kuna haja ya kuwepo lugha ya kuwawezesha kuwasiliana. Kama ilivyo katika nchi jirani za Kenya na Tanzania lugha ya Kiswahili imewaunganisha. Serikali ya Uganda kupitia sera ya lugha inafaa kupitia elimu kufundisha Kiswahili kwa kila raia ili mawasiliano yawepo katika nchi nzima kwa kutumia Kiswahili. Hili halitatuji suala la mawasiliano tu bali pia litasaidia kuondoa ugonjwa wa ukabila uliyomo nchini Uganda.

Katika uendelezaji wa upangaji lugha, msingi huu unazungumzia juu ya jambo la hadhi ya lugha kama lilivyozungumziwa na (Heinz Kloss na William Stewart 1968) ambao walizungumzia juu ya sifa nne zinazoeleza hadhi ya lugha ikiwa ni pamoja na:

Chimbuko la lugha, ikiwa lugha hiyo ilianzia pale inapozungumzwa au ni lugha ngeni, kiwango cha usanifishaji na kiwango cha kisarufi kinachoifanya itumiwe vizuri. Miongoni mwa masuala yanayoshughulikwa hapa ni kabaini kukubalika kwa lugha hiyo kisheria kwa muktadha huu Kiswahili kinakubalika kisheria kama ilivyoielezwa

hapo awali. Suala jingini ni kama ikiwa ni lugha rasmi, ni lugha rasmi katika nchi ambako kuna lugha nyingine rasmi? Katika kujibu swali hili ni kwamba katiba imeliweka wazi kama ilivyoilezwa hapo juu kwamba Kiswahili itakuwa lugha rasmi ya pili, kwa maana kwamba kuna lugha rasmi ya kwanza nayo ni Kiingereza. Swali jingine linaloibuka kuhusiana na maoni ya Kloss na William (wameshatajwa), ni je, Kiswahili ni lugha ya jamii au jumuiya fulani? Katika kujibu swali hili, Kiswahili ni lugha ya jumuiya ya Afrika Masharika ambapo Uganda ni mwanachama. Hili linafuatwa na maswali kama je, Kiswahili ni lugha inayotumiwa katika mikakati ya kijamii lakini haitambulishwi kisheria? Jibu la swali hili ni kwa pande mbili.

Moja ni kwamba ni kweli Kiswahili hutumiwa katika masuala ya kijamii kama biashara lakini mbali na mapendekezo katika katiba kwamba itakuwa lugha rasmi ya pili. Pili, ni kwamba hakuna sheria zaidi na pendekezo la kuifanya lugha rasmi ya pili ambalo limebaki kwenye karatasi bila kutekelezwa. Maswali yanaendelea kuibuka kama, Kiswahili ni lugha ambayo hairuhusiwi kutumiwa au ni lugha ya kidini? Kwa kweli hakuna anayekatazwa kuitumia katika serikali, ila katika shule nyingi inachukuliwa kama lugha ya kawaida isiyoruhusiwa kutumiwa. Vilevile, pamoja na kwamba watu wengi hawajafundishwa kuitumia ikitumiwa afisini au hata katika masuala ya kijamii mengine, wasikilizaji wengi watadai kutoelewa msemaji. Kuhusiana na suala la kidini, kuna wanaodai kwamba Kiswahili ni lugha ya Kiislamu ila haijaoneshwa kisheria kwamba Kiswahili ni lugha ya kidini.

Katika makala haya tumeangalia utekelezaji wa sera zinazohusiana na Kiswahili na utekelezaji wa sera hizo. Kwa mfano katiba ya Uganda inapopendekeza kwamba Kiswahili iwe lugha rasmi ya pili ya nchi, hili linafaa kutekelezwa kwa kuwafanya wanafunzi wafundishwe nchini kote. Ingawa Kiswahili nchini Uganda kimekubalika kisheria kama lugha rasmi ya pili, hili halijatekelezwa kikamilifu.

Naye Stewart (1968) anazungumzia vitengo vya upangaji lugha ikiwa ni pamoja na lugha rasmi, lugha ya kimkoa, lugha inayozungumzwa na watu wengi, lugha ya kitaifa, lugha ya jiji au kimji, lugha ya kikundi au ya kikabila, lugha ya kielimu, lugha inayofundishwa kama somo, lugha ya kifasihi au inayotumiwa na wasomi. Kutokana na maoni ya Stewart (keshatajwa) tunakiri kwamba Kiswahili ni lugha inayofundishwa kama somo nchini Uganda lakini kama ilivyo, elimu ni suala la kiusawa ambapo kila mtu anafaa afaidike. Pamoja na kwamba Kiswahili ni lugha inayofundishwa katika baadhi ya shule fulani haifundishwi katika shule zote nchini wala serikali haijatoa ushauri kwamba ifundishwe popote. Kwa mfano shule zinazofundisha Kiswahili ni zile kutoka Magaharibi mwa Uganda na wala siyo zote na nyingine chache kutoka kati mwa Uganda. Mashariki na Kasikazini mwa Uganda Shule zinazofundisha Kiswahili ni za kuhesabia kwenye vidole tu. Mbali na hitilafu hizo, Serikali haijatoa kauli yoyote kufidia hitilafu hiyo.

Kuhusiana na nadharia ya upangaji lugha, makala haya yalitumia muhimili wa nadharia ya uchaguzi na utekelezaji kwa kutumia muhimili wa tatu ambao unazungumzia juu ya majukumu ya viongozi. Kutokana na Kaplan na Baldauf (1997)

wanaeleza kwamba jukumu la viongozi ni pamoja na kuhakikisha kwamba mambo yafuatayo sita yanatimizwa ambayo ni:

Kuamua ni lugha ipi ambayo itafundishwa katika mtalaa wa kielemu.

Kubaini kwamba walimu wamefuzu kwa kiwango gani.

Kuhusisha wanajamii.

Kuamua ni vifaa gani vitakavyotumiwa na kwa kiwango gani na katika silabasi ipi?

Kuanzisha jinsi au mfumo utakaotumiwa kutathimini maendeleo ya lugha.

Kubaini gharama itakayotumiwa.

Pamoja na maoni hayo kama yanavyotolewa na Kaplan na Baldauuf (wameshatajwa) kama wanavyorejelewa na Nahir (2013), makala haya yamebaini kwamba pamoja na kuweco kwa viongozi wa kisiasa na kielimu, kubaini kwa masomo ya kufundishwa kupo. Kwa mfano gazeti la *Newvision* la Novemba 21 2017 lina orodho ya masomo ambayo yaliorodheshwa ikionyeshwa kwamba lugha ya Kiswahili imo miongoni mwa masomo yanayofaa kufundishwa katika shule za upili. Ikumbukwe kuwa kuwapo kwa masomo hayo haimaanishi kwamba Kiswahili ni somo la lazima ina maana kwamba mwanafunzi anaweza kulisoma au asilisome. Kwa nini tuseme hivyo? Kumekuwepo mapendekezo ambayo yameundwa na shirika la uandaaji mitalaa la NCDC ambayo yanaonesha kuwa Kiswahili ni lugha ya lazima katika shule za upili (CURRASSE, 2013). Mapendekezo haya yamesainiwa na aliyekuwa waziri wakati huo Mheshimiwa. Meja mstahafu Jesca Alupo lakini raisi wa nchi Mheshimiwa Museveni alisitisha utekelezaji wa sera hii kwa madai kwamba kuna wadau wengine wa kielimu waliopinga.

Kuhusiana na kubaini kwamba walimu wa kufundisha somo fulani wamefuzu, Prof, Emanuel Karoro aliyekuwa mkuu wa Chuo cha Kitaifa cha Kakoba (NTC Kakoba) alipoona mapendekezo ya “*Government White Paper on Education*, alianzisha ufundishaji wa Kiswahili kwa kiwango cha astashahada na stashahada na vyeti katika Kiswahili. Uanzishaji huo ulichangia pakubwa katika kutoa walimu wa Kiswahili. Baadaye uongozi wa Chuo Kikuu cha Makerere ulifufua tena ufundishaji wa Kiswahili (ambao ulikuwepo miaka hapo zamani kama ilivyotajwa hapo awali lakini kikasitishwa kwa ajili ya viongozi kutokitilia maanani) kwa kiwango cha shahada, Chuo Kikuu cha Kyambogo nacho kilianzisha mnamo mwaka wa 2003, ikafuatwa na vyuo vingine vya kibinafsi. Kwa upande wa viongozi wa vyuo wamejaribu iwezekanavyo kwa mfano Chuo Kikuu cha Kyambogo kinatahini Kiswahili kwa kiwango cha walimu wanaosoma kozi ya ualimu wa shule za msingi, wanapohitimu wanapata astashahadi ya kiwango cha tatu kama walimu (*Grade three teachers*) na pia kinatahini Kiswahili kwa kiwango cha walimu wanaofanya kozi ya kufundisha Kiswahili wanaohitimu na stashahada. Mbali na hilo, kozi kama shahada ya udalisi na wale wanaohitimu kufundisha katika shule za upili zipo na kiswahili ni mojawapo ya karatasi za lazima wanazozifanya kwa kiwango cha astashahada na stashahada kwa wale wanaojifunza kozi ya ufundi.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu nchini Uganda nao umeanzisha ufundishaji wa Kiswahili kwa kiwango cha umahiri/uzamili jambo ambalo limechangia katika uimarishaji wa utaalumu katika Kiswahili. Tofauti na hayo, Chuo Kikuu cha Makerere

kimeanzisha shahada ya uzamili katika isimu lakini haijasaidia sana katika uendelezaji wa Kiswahili kwa sababu kozi zinafundishwa kwa Kiingereza na tasnifu ingawa zinahusu Kiswahili lakini wanafunzi wanashauriwa kuziandika kwa Kiingereza. Hii ni changamoto kubwa kwa wanafunzi na uongozi wa chuo haujalitaua. Hapo mwanzoni, tasnifu ziliandikwa kwa Kiswahili lakini tena uongozi ukabadilisha. Hili limechangia katika kupunguza idadi ya wanafunzi wanaofanya kozi ya uzamili katika Kiswahili kupitia Chuo Kikuu cha Makerere.

Kuhusiana na suala la kuhusisha wanajamii, serikali haijahusisha wanajamii katika kuendeleza Kiswahili. Kwa maoni yetu kutokuwepo kwa lugha ya taifa kama ilivyo katika nchi ya Tanzania na Kenya ambapo Kiswahili ndiyo lugha ya taifa inaifanya jamii ya Uganda kutotilia maanani Kiswahili. Inakuwa kana kwamba jamii ya Uganda isipokuwa wale wachache wanaozungumza Kiswahili, wengine hawaoni sababu ya kujifunza Kiswahili kwa sababu serikali yenyewe haijakitilia maanani. Linalofaa kufanywa hapa ni kwamba viongozi wa kidini, kisiasa, kielimu na viongozi wote nchini Uganda wanafaa kuhusisha jamii katika shughuli za kijamii kwa kutumia Kiswahili. Jambo linaloshangaza ni kwamba katika masuala hata sherehe za kitaifa mbali na kuwa Kiswahili ni lugha rasmi ya pili nchini Uganda, lugha inayotumiwa mara nyingi huwa ni Kiganda na Kiingereza. Labda jambo la kudokeza hapa ni kwamba nchini Uganda siku hizi kuanzia mwaka wa 2013 na kuenda mbele sasa sherehe nyingi zinazokusanya jamii, wimbo wa jumuiya unaimbwa kwa Kiswahili wala hakuna kiingine kinachoendelea kwa Kiswahili.

Hilo ni jambo la kushangilia na kupendekeza kwamba viongozi wasikome katika wimbo tu bali pia wahusishe jamii katika kuishauri kusoma Kiswahili na siyo kuisoma tu hata wale wasioweza kuipata kupitia shule kujifunza kwa njia zozote zile muradi tu wanaweza kuiongea. Mfano wa jamii kuhusiana na Kiswahili ni jamii ya Waganda ambao wengi wao hawaruhusu watoto wao kujifunza Kiswahili. Viongozi wanafaa kuchukua jukumu la kuwahamasisha kwa njia ya kuwashawishi na kuwaelezea umuhimu wa Kiswahili.

Kwa kuzingatia muhimili wa viongozi kuamua ni vifaa gani vitakavyotumiwa na kwa kiwango gani na katika silabasi. Viongozi ambao makala haya yameangalia ni wale wa kisiasa ambao wanafaa kulipia vifaa kama vitabu vya kiada na ziada. Hali ilivyo nchini Uganda, pamoja na kuwa kuna kubadilisha vitabu vya fasihi katika mchepuo wa kidato cha tano na cha sita, viongozi wa mitaala wanachofanya ni kutoa orodha ya vitabu wala viongozi wa serikali hawajishughulishi na kununua vitabu hivyo na visambazia katika shule zote nchini. Hata kwa shule za serikali jukumu hili limeachiwa wanafunzi na wazazi. Hata hivyo makala haya yanatambua kwamba kuna baadhi ya viongozi wa shule ambao wamejitolea kununua vitabu ingawa wakati mwingine havitoshi. Si kwa mchepuo wa kidato cha tano na cha sita tu bali pia kuanzia kidato cha kwanza hadi cha tano hadithi ndiyo hiyo hiyo. Tafauti na shule za upili, shule za msingi za serikali, uongozi wa wizara ya elimu wamesambaza vitabu katika shule hizo lakini serikali yenyewe haijaajiri walimu wa kufundisha katika shule hizo.

Kuhusu suala la kuanzisha jinsi au mfumo utakaotumiwa kutathimini maendeleo ya lugha, makala haya yanatambua kwamba kumekuwepo mfumo bora kwa mfano uongozi mkuu wa NCDC wa kutoe mapendekezo ya kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima ulikuwa mfumo mzuri. (CURRASSE, 2013). Vile vile uamuzi wa tume ya Kajubi (1989), na baadaye “*Government White Paper on Kiswahili*” haya yote ni shughuli zinazonuia kuendeleza Kiswahili. Shirika la uandaaji wa mitihani UNEB vilevile linaajibika kwa kutunga mitihani ya Kiswahili. Lakini uongozi wa serikali haujashabiki mazoezi ya kuendeleza Kiswahili kuhusiana na mashirika ambayo yametajwa katika aya hii. Kwa mfano shirika la UNEB limetoa mpango mkakati unaonyesha kwamba mwaka 2019 Kiswahili kitaanza kutahiniwa katika darasa la saba, lakini waziri wa elimu na viongozi wa shule hawajaweka mfumo wowote wa kujitayarishia au hata kutayarisha wanafunzi kwa mtihani huo. Makala haya yanatambua kwamba ni udhaifu wa viongozi kwa kutotekeleza sera kufundisha Kiswahili katika shule za msingi.

Hitimisho

Mwishoni mwa yote, serikali ya Uganda ikilinganishwa na Nchi ya Tanzania na Kenya kuhusiana na sera ya lugha hasa Kiswahili pamoja na utekeleza wa mapendekezo yanayoniua kuendeleza Kiswahili, bado inahitaji kujikakamua na kuwajibikia suala hilo. Hili linaweza kufanyika kwa kufadhili wasomi wa Kiswahili, kuajiri walimu waliopo, kugharamia vifaa vya kufundishia Kiswahili, kuhakikisha kwamba Kiswahili kinafundishwa nchini kote pamoja na kuhakikisha kwamba mapendekezo yanayoniua kuendeleza Kiswahili yanafanyiwa kazi kupitia sera. La sivyo, Uganda itabaki nyuma katika uendelezaji wa Kiswahili.

Marejeleo

- Mazrui, A. A. na Mazrui, A.M. (1995). *Swahili State and Society*. The Political Economy of an African Language. East African Educational Publishers.
- Haugen, E. (1987). *Language Conflict and Language Planning*. Cambridge, Mass. Harvard University Press.
- Jjingo, C. na Visser, M.(2017). The Senteza Kajubi Legacy: The Promotion of Teaching Kiswahili in Uganda. *Africology. The Journal of Pan African Studies*. Juzuu. 10(9), 1-10.
- Kaplan, R. B. na Baldauf, J. R. B. (1997). *Language Planning from Practice to Theory*. Clevedon: Multilingual Matters Ltd.
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. 2nd Edition, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mpuga. D. (2003). *The Official Language Issue. A look at the Uganda Experience*. A paper presented at the African Language Research Project Summer Conference Ocean City, Maryland. Haijachapishwa.
- Mugaga, (2010) *Why Kiswahili Teaching Remains Difficult*. Haijachapishwa.
- Mukama, R. (2009). Theory and Practice in Language Policy: The case of Uganda. Kiswahili, University of Dar es salaam: *Jarida la Kiswahili*. Juzuu: 72(1):68-107.
- Nahir, (2003). "Language Planning Goals: A Classification." *Sociolinguistics: The Essential readings*. Eds. Paulston, Christina Bratt and G. Richard Tucker. Oxford: Blackwell.
- Nankindu. P., Kirunda. R. na Ogavu. T. (2015). Language in Education in Uganda: The Policy, the Actors and the Practices. A case of Urban Districts of Kampala. *Indian Journal of Research. Peripex*. Juzuu 4(5):190-193.
- Nsibambi, N. (1971). *Language policy in Uganda: An investigation into costs and politics*. Makerere Univeristy. Haijachapishwa.
- Rusekampunzi, E. (1988). Language Policy and the Development of Kiswahili in Rwanda. Tasnifu ya uzamili katika Isimu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Haijachapishwa.
- Ssekamaanya, S. S. (2017). Sababu za kuhitilafiana kwa sera na utekelezaji wake katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda wilayani Luwero. Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kiislamu nchini Uganda. Haijachapishwa.
- Stewart, W. (1968). "Sociolinguistic Typology of Multilingualism". Readings in the Sociology of Language. Ed. Joshua Fishman. The Hague. Mouton Publishers.
- Tembe, J.H. (2008), Language Education policy and Multilingual Literancies in Ugandan primary schools. A PhD thesis. The University of British Columbia. Haijachapishwa.
- Viera, P. (1996). *Swahili and the Dilemma of Uganda language policy*. Asian and African Studies. Institute of Orient and African studies, Slovák Academy of Sciences, Klemensova 19,813, 63 Bratislava, Slovakia.